TANGAZO LA SERIKALI Na. 805 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA UKIRIGURU YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Ukiriguru ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

*Tangazo la Serikali Na. 805 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV152 yenye majira – nukta 499470.607MS, 9699049.288KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo KS141°11’40”KS kwa umbali wa kilomita 0.06 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV151 yenye majira – nukta 499885.528MS, 9698628.296KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS135°52’50”KS kwa umbali wa kilomita 4.25 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV153 yenye maira - nukta 502834.058MS, 9695562.784KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo KZ256°13’40”MS kwa umbali wa kilomita 2.92 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV362 yenye majira – nukta 505664.791MS, 9696263.974KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea KAskazini - Mashariki katika uelekeo wa MS218°26’00”MS kwa umbali wa kilomita 1.33 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV53 yenye majira – nukta 506512.367MS, 9697290.580KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ231°11’10”MS kwa umbali wa kilomita 1.23 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV194 yenye majira – nukta 507304.986MS, 9698228.934KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS220°51’00”MS kwa umbali wa kilomita 3.59 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV170 yenye majira – nukta 509766.048MS, 9700854.066KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa KZ155° 05’50”KZ kwa umbali wa kilomita 3.03 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B10 yenye majira – nukta 509554.161MS, 9701386.311KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata mto Nyamatara hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV167 yenye majira – nukta 508822.641MS, 9703315.127KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata mto Nyamatara hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV18 yenye majira – nukta 506113.081MS, 9706848.975KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS219°16’30”MG kwa umbali wa kilomita 4.34 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV69 yenye majira – nukta 503449.323MS, 9703725.304KZ. Baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS203° 59’20”MG kwa umbali wa kilomita 2.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV163 yenye majira – nukta 502464.899MS, 9701510.349KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa MG249°39’30”MG kwa umbali wa kilomita 1.65 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KV261 yenye majira – nukta 500947.244MS, 9700854.066KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS218°38’00”MG kwa umbali wa kilomita 2.31 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*